

Public education  
Discover a world of opportunities

## KUANDIKA NA KUTAMKA HERUFI: KUSOMEA NYUMBANI

### KUANDIKA NA KUTAMKA HERUFI NI MHIMU!

Kuzungumza na kusikiliza misingi ambayo maandishi, herufi na kusoma hujengwa kwayo. Mtoto wako anaendeleza haya na ujuzi mwingine wakati wanahudhuria Chekechea. Wakati wanajenga maneno yao na kusikiliza kwa kujiamini, wanaanza kujifunza kuhusu uandishi.

#### Naweza kufanya nini?

- Soma na mtoto wako mara kwa mara. Chunguza maneno na vitabu pamoja na kuwashirikisha wakati unaandika.
- Unaposoma pamoja, zungumza juu ya maneno unayoyasoma. Kwa mfano, sauti ya maneno kama: *bat* na *cat*, na zungumzia sauti zilizofanywa mwanzoni mwa maneno.
- Himiza mtoto wako kukusaidia kuandika maelezo, barua pepe na orodha ya ununuzi Andaa karatasi na penseli ili waweze kujaribu kuandika na wewe.
- Cheza michezo ya maneno kwa pamoja kama vile kulinganisha jina la mnyama kwa picha.
- Onyesha herufi na michoro ambayo mtoto wako ameiunda. Andika maelezo kama : *Nafurahia sana kwa ajili yako!*

**Kama mtoto wako anazungumza lugha nyingine au ulimi, wanahitaji mda ili kusikia sauti ya lugha ya Kiingereza. Inaweza kuchukua hadi miaka miwili au zaidi kwa wao kusikia na kusema sauti hizi zote.**

**Zima televisheni. Ni rahisi mtoto kuweza kutulia kama hakuna vitu vya kumkatiza.**

- Msaidie mtoto wako kutambua majina yake. Anza kwa kuwataka kusikiliza sauti ya kwanza katika jina lake.
- Zungumzia kuhusu herufi ya kwanza ya jina lao. Watia moyo kuangalia herufi hiyo katika maeneo mengine. Kuwasaidia kuandika herufi za jina lao.
- Wakati unaandaa chakula cha jioni uliza maswali kama vile: *Je, unaweza kupata kitu jikoni ambacho huanza na sauti sawa na jina lako?*
- Kutumia muda pamoja kuangalia kwa herufi na maneno ya mtoto wako anayoyajua. Unaweza kufanya hivyo nyumbani, katika gari, katika maduka na kwenye uwanja wa michezo.
- Fanya kusoma kuwa kwa kufurahisha!

**Mtoto mlemavu kwa kawaida anafaidika na kufurahia kutokana na mwingiliano wa karibu na kulisimua unaotolewa wanapokuwa wakisoma hadithi zao wanazozipenda au nyimbo zinazoimbwa za kitalu. Kama mtoto wako ana ulemavu, shule zao zinasaidia wao kwa wao kushiriki katika shughuli katika ngazi zinazofaa kwa uwezo wao. Kuzungumza na mwalimu wa mtoto wako kuhusu zana sahihi, vifaa na mawazo ya kusaidia wewe na mtoto wako.**



Department of  
Education

Utajua zaidi  
Kijitabu cha ukweli wa kusomea nyumbani  
Kwenye [education.wa.edu.au](http://education.wa.edu.au).